

Swahili

Mradi Makini wa Lugha ya Kiingereza

Kijitabu cha Habari kwa Wazazi



The Pines School

Jina la shule:

The Pines School

Anwani:

42 Andrew Smith Drive, Parafield Gardens 5107

Simu:

(08) 8281 2199

Barua pepe:

Priyanka.Sharma459@schools.sa.edu.au

**Nambari ya simu
kuwasiliana:**

(08) 8281 5906



Government of South Australia

Department for Education and
Child Development

Karibu kwa **The Pines School**

Timu ya Uongozi wa Shule



Cherie Collings
Principal



Sam Konnis
Deputy Principal



Priyanka Sharma
Assistant Principal, IELC

Kuhusu Mradi Makini wa Lugha ya Kiingereza na Mradi wa Wapya Waliowasili katika Australia Kusini

Idara ya Elimu na Maendeleo ya Watoto inatoa msaada makini wa lugha ya Kiingereza kwa wanafunzi wapya waliowasili nchini Australia. Katika shule za msingi, mradi huu unaitwa Mradi Makini wa Lugha ya Kiingereza (Intensive Kiingereza Language Program) (IELP) na katika shule za sekondari, unaitwa Mradi wa Wapya Waliowasili (New Arrivals Program) (NAP).

Wanafunzi wa usuli wa ukimbizi na uhamiaji hujiandikisha katika kituo cha IELP au NAP kabla kuanza kujifunza katika shule za kawaida. Kuna vituo kumi na saba vya msingi, kituo kimoja cha sekondari na kituo kimoja cha sekondari juu. Wanafunzi wa shule za msingi hujiandikisha kwenye kituo cha karibu sana kwa nyumbani kwao. Ikiwa unahamia kwa anwani mpya, inaweza kumaanisha mtoto wako atahitaji kwenda IELP katika shule nyingine.

Sababu

IELP/NAP inatoa nafasi kwa wanafunzi:

- Kuandaa kwa shule ya kawaida
- Kujifunza Kiingereza kwa makini kwa maeneo mengi ya mtalaa katika madarasa madogo
- Kujifunza kuhusu na kushiriki katika mashughuli ya utamaduni wa Australia
- Kupokea msaada katika lugha ya kwanza, inapowezekana
- Kuzidi matumaini kuishi katika jamii ya Australia.

Kwa habari zaidi, omba shule kwa kifurushi cha IELP/NAP, kinachopatikana kwa lugha 20.

Muda wa Kukaa

Muda wa kukaa na IELP/NAP unategemea na kiasi gani cha elimu ya shule mtoto wako ameshafanya na ustadi wake wa Kiingereza alipowasili. Kawaida wanafunzi wa msingi wanaendelea na IELP kwa muda wa miezi 12–18. Wanafunzi wa sekondari wanaweza kuendelea kwa miezi 12–24.

Kuwekwa Darasani

Wanafunzi wanawekwa katika madarasa ya daraja ya mwaka inayofaa kwa umri wao. Kutakuwepo wanafunzi wamo darasani na madaraja mbalimbali ya Kiingereza lakini kwa karibia umri mmoja. Ni muhimu kwamba watoto wapate marafiki wanaoweza kuhusiana.

Mabadiliko

Wakati mwanafunzi yupo tayari kuingia darasa la kawaida, wafanyakazi wa shule watasaidia mabadiliko kwenda shule mpya. Kawaida hii itakuwa kwa shule ya mtaa wake. Angalau tembezi moja litapangiliwa kwenda shule mpya. Mara tu mtoto wako anapoanza kwenda shule mpya, mwongozi wa IELP/NAP atapeleka taarifa ya kuondoka yenye habari kwa mwalimu mpya.

Mtalaa



Mtalaa wa IELP NAP una fokasi wa nguvu kwa mahitaji ya lugha ya maeneo tofauti ya kujifunza katika mtalaa wa Australia kama hisabati, afya au jeografia. Walimu wanaelewa kuhusu mfuatano ya maendeleo ya lugha ya Kiingereza na wanatarisha wanafunzi kwa mahitaji yao ya mawasiliano ya kijamii pamoja na kujifunza yote ya mtalaa. Kwa sababu wanafunzi wapya wanaweza kuanza wakati wowote katika muhula, walimu wanatoa mradi wa lugha ya Kiingereza unaofaa kwa mahitaji ya kujifunza kwa wakati ule wa kuingia darasani.

Uchaguzi wa mtalaa hufanyikiwa kwa uangalifu kwa sababu kuna muda fulani tu katika mradi huu. Walimu wanapanga kazi za kujifunza ambazo zitasaidia wanafunzi katika mabadiliko yao kwenda madarasa ya kawaida.

Kufundisha na Kukadiria

Hapo Australia Kusini, walimu wamo IELP/NAP wana ustadi mengi wa kufundisha Kiingereza kama lugha ya kuongeza. Wanaelewa kwamba uzoefu wa mtoto wako wa shule unawezekana kuwa tofauti sana na matazamo ya shule nchini Australia. Walimu watasaidia wanafunzi kuchangia katika mazungumzo ya darasa, kuuliza maswali, kufanya kazi kwa timu na kufikiria kwa kubuni.

Walimu wote wanatumia kifaa cha kukadiria, *Madaraja ya Lugha na Kujua Kusoma na Kuandika (Language and Literacy Levels)* kufundisha Kiingereza na kukadiria mafaniko ya wanafunzi. Maendeleo ya mtoto wako yanarikodiwa kila muhula. Katika IELP ya msingi, walimu hutumia Ripoti ya Maendeleo na Ripoti ya Hisabati na Kujua Kuhesabu kukumbuka walichojifunza.



Maafisa wenye Lugha Mbili wa Huduma za Shule

Maafisa wenye Lugha Mbili wa Huduma za Shule (Bilingual School Services Officers) (BSSO) wanasaidia kutulia na maendeleo ya lugha ya Kiingereza ya wapya waliowasili. Wanasaidia wanafunzi kwa mmoja mmoja au katika vikundi vidogo. Wanasaidia pia na mawasiliano kati shule, wanafunzi na wazazi. Shule wanaamua maamuzi kila muhula kuhusu msaada wa lugha ya kwanza ambao wanafunzi wanaohitaji. Msaada huu unategemea upatikanaji wa BSSOs.

Matembezi na Matukio ya Shule

Matembezi na kushiriki katika matukio ya shule husaidia wanafunzi kujifunza kuhusu jamii ya mtaa na jumuiya nzima na ni sehemu ya mtalaa wa IELP/NAP. Uzoefu huu ni nafasi ya kufahamu zaid mazoezi ya utamaduni na kupata lugha inayohitajika kushirikia.

Usafiri

Wanafunzi wanaokuwa na umri chini wa miaka 10 na wanaoishi mbali zaidi ya kilomita 1.75 kutoka shule wanaweza kustahili kusafiri kwenda na kutoka shule kwa daladala.

Usalama wa wanafunzi katika daladala ni wajibu wa kushiriki.

Wajibu ya walezi:

- Kuhakikisha wanafunzi wapo tayari na kungoja basi asubuhi
- Kuwepo nyumbani na aonekane wakati wanafunzi wanaposhusha mchana
- kuongea na mtoto wako kuhusu umuhimu wa matendo mazuri
- kufahamisha shule au dereva kama usafiri hauhitajiki kwa siku fulani.

Wajibu ya wanafunzi:

- kufuata mafunzo ya dereva
- kufunga kanda la kiti na vaa wanaposafiri
- kuongea kwa sauti ndogo
- kuacha kula au kunywa
- kuacha kusimama au kubadilisha viti
- kutoweka sehemu yoyote ya mwili nje ya dirisha.

Madereva huripoti wanafunzi ambao hawafuati masheria hayo. Ikiwa matendo yanaendelea, au ikiwa ni mno, mtoto hataruhusiwi kusafiri kwa basi kwa siku moja angalau. Wazazi watafahamishwa. Kwa sababu yule mwanafunzi hajasimamishwa kwa muda, itakuwa wajibu ya mlezi kusafirisha mwanafunzi kwenda na kutoka shule.

Habari za Shule

Wakati wa Shule

Jumatatu-Ijumaa
{Monday – Friday}

08:50 am – 03:00 pm

Wakati wa Kengele

Wakati	Shughuli
08:30 am	Wanafunzi wanaweza kuingia viwanja vya shule
08:40 am	Shule inaanza
08:50 am	Masomo
10:40am	Kipindi cha kupumzika
11:00 am	Masomo
12:40 pm	Kula chakula cha mchana
12:50 pm	Kipindi cha kupumzika mchana
01:20 pm	Masomo
03:00 pm	Mwisho wa siku ya shule

Mahudhurio/Kutokuwako

Kwa Australia Kusini, wanafunzi wote kati ya umri wa 6 na 17 wanahitajika kwa kisheria kwenda shule kila mara. Mahudhurio kila mara na kushiriki hai katika miradi ya elimu ni lazima kwa mafaniko ya kitaaluma.

Ikiwa mtoto hayupo shuleni, ufahamisha shule kwa njia ya simu au maandishi.

Ikiwa unajua kwamba mtoto wako hatakuwepo kwa siku 3 au zaidi kwa sababu ya mambo ya familia, fomu ya kusamahewa **lazima** ijazwe na kukubaliwa na Mwalimu Mkuu, kabla yeye kuondoka.

Kuchelewa Kuja au Kuondoka Mapema

Mwanafunzi anayechelewa kuja:

- lazima aende ofisi ya mbele na kukusanya karatasi ya kuchelewa kabla kwenda darasani.
- lazima aende darasani mara moja.
- lazima aende ofisi ya mbele na weka sahihi karatasi ya kuchelewa kuja.
- lazima weka sahihi kwa Ofisi ya Mwanafunzi.

Kwa mwanafunzi anayehitaji kuondoka mapema:

- mzazi/mlezi lazima aweke sahihi kwenye kitabu kwenye ofisi ya mbele.
- mzazi/mlezi lazima uandike kumbusho katika kitabu cha kumbukumbu cha mtoto wako.
- mzazi/mlezi lazima upate karatasi ya mapema kutoka ofisi ya mbele na ichukue kwa mwalimu wa darasa.
- mzazi/mlezi lazima aongee na mwalimu wa darasa ya mtoto wako.
- weka sahihi kuondoka pale Ofisi ya Mwanafunzi.

Kusimamia Kiwanjani

Wanafunzi wasikuwepo shuleni kabla ya **08:30 am** or baada ya **03:20 pm** kwa sababu mwalimu hayupo kuwaangalia.

Afya na Usalama wa Wanafunzi

Mazingira ya Usalama wa Watoto

Walimu wanaelewa wanafunza wanahitaji kujihisi salama. Wanafundisha wanafunzi kuhusu hali, vitu na matendo yenye hatari. Uonevu hauvumilii, popote darasani au kiwanja cha kuchezea, au kupitia media ya tarakimu.

Wazazi na walimu wana wajibu kulinda watoto kuzuia hatari kwa usimamiaji wa kufaa wakati wanapotumia teknolojia.

Shule na wafanyakazi wao wanahitajika na kisheria kutoa repoti kuhusu matusi na uzembe wa shaka wa mtoto kwenye Laini ya Ripoti ya Matusi ya Mtoto.

Utaratibu wa Dharura

Shule zote zinatumia utaratibu wa dharura ili wanafunzi wanafahamu kufanya nini ikiwa kiwanja au majengo si salama. Wakati wa *kuhamisha (evacuation)*, wanafunzi wanatoka majengo na kukutana pamoja kiwanjani, nk mazezi ya utaratibu ukitokea moto. Wakati wa *kuhama (invacuation)*, wanafunzi wanatoka kiwanja na wanapata salama ndani majengo.

Wageni wanaombewa kujaza 'Kitabu cha Wageni' pale Ofisi ya Mbele. Ndipo wafanyakazi wanajua nani yupo shuleni kama dharura ikitokea.

Chawa ya kichwa

Chawa ya kichwa ni kawaida katika wakati fulani ya mwaka. Wafanyakazi wataangalia nyewe za mtoto wako kama kuna mlipuko, na ruhusa yako. Wakati chawa ya kichwa wanapogunduliwa, familia zote wa darasa lile watafahamishwa ili unaweza kuangalia nyewe za mtoto wako pale nyumbani. Wanafunzi wakae nyumbani mpaka shampu ya tiba imetumiwa na mayai yote yameondelewa.



Kuangalia kwa Chawa ya Kichwa

Hali ya Hewa ya Joto au yenye Mvua

Kwa siku za joto kabisa au hali ya mvua, wanafunzi wanabaki ndani wakati wa vipindi vya mapumziko na chakula cha mchana, chini ya usimamiaji wa walimu.

Kuumwa/Jeraha

Watoto wagonjwa wakae nyumbani ili magonjwa hayaambukizi wengine. Ikiwa hawapo shuleni, ufahamishe shule. Wanafunzi wanapopata ajali au wakiumwa pale shuleni wanaletwa Ofisi ya Mbele/ chumba cha magonjwa. Wanafunzi wanatunzwa na ikihitajika, walezi wanaweza kupigwa simu kuomba wamsindikize nyumbani. Kwa majeraha au ugonjwa mkali ambulensi inaweza kuja.



Nyenzo za chuma cha Mgonjwa

Magonjwa ya Kuambukiza

Katika miaka michache ya kwanza shuleni mtoto anaweza kupata maambukizo mbalimbali. Ili wengine wawe salama, wanafunzi wanahitaji kukaa nyumbani wakati wanapoumwa. Vipindi vya kutengwa vinavyoonyeshwa chini ni vipindi vya chini kabisa. Daktari yako atahakikisha muda gani mtoto wako atahitaji kupumzika nyumbani.

Mgonjwa	Kipindi cha Kutengwa (muda kukaa nyumbani)
Tetekuwanga	Siku 5 kuanza kujitokeza madoa
Macho mekundu (Ugonjwa wa shavu nyekundu)	Tenga mpaka hakuna kutoka usaha machoni
Homa ya Tezi	Usirudi mpaka mtu anajisikia vizuri
Mkono, Mguu na Mdomo	Tenga mpaka lengelenge yote imekauka
Upele ambukizi wa malengenge (vidonde vya shule)	Tenga mpaka matibabu yanayofaa yameanza. Madonda ya wazi yafunikwe
Homa ya mafuna na mafua	Usirudi mpaka mtu anajisikia vizuri
Surua	Siku 4 kuanzia kujitokeza vipelele
Matumbwitumbwi	Siku 9 au mpaka uvimbe unapopunguza
Choa	Tenga mpaka siku moja baada matibabu yameanza
Rubela (Surua ya Ujerumani)	Siku 5 kuanzia kujitokeza vipelele
Upele	Tenga mpaka siku moja baada matibabu yameanza
Kifaduro	Tenga kwa siku tano baada ya kuanza matibabu ya antibiotik

Madawa

Walezi wanaombewa kutoa habari na matibabu ya sasa-hivi kwa magonjwa na mzio, pamoja na pumua kwa Ofisi ya Mbele. (Mpango wa Matibabu wenye sahihi, uliojazwa na daktari unahitajika kwa wanafunzi wanaohitaji madawa ya kila mara).

Wafanyakazi hawawezi kuwapa wanafunzi wagonjwa dawa yoyote, hata Panadol. Hata hivyo, wafanyakazi wenye mafunzo wanaweza kusaidia au kuwasimamia wanafunzi kutumia madawa yao wenyewe.

Huduma ya Meno ya Shule

Huduma ya Meno ya Australia ya Kusini inatoa utunzaji wa meno kwa watoto wote chini ya umri wa miaka 18. Huduma hii ni bure ikiwa una:

- Kadi ya Kipunguzo cha Centrelink
- Kadi ya Shule
- Ratiba ya Posho ya Meno ya Mtoto.

Kama mtoto haitunzwi na mmojawapo ya hiyo, kutunza meno kwa jumla au dharura kutagharimia ada ndogo. Tafadhali piga simu zahanati chini kupata miadi. Siyo zahanati zote zinafungua kila siku.

Jina la zahanati ya mtaa:

Salisbury Downs Dental Clinic

Anwani:

Hollywood Boulevard, Hollywood Plaza Shopping Centre, Salisbury Downs

Simu:

(08) 8250 9254

Wakati wa dharura, piga simu kwenye 1800 022 222.

Kupima Kifua Kikuu

Zahanati ya Kifua ya Hospitali ya Royal Adelaide (RAH) inatembelea vituo vya IELP kila mwaka kupima kwa kifua kikuu (tuberculosis) (TB). Hiki ni ugonjwa wa vipafuu, na ni kawaida katika nchi nyingi za ng'ambo. Vijana kutoka maeneo ya hatari kubwa wana uwezekano mkubwa zaidi wa ambukizo na ugonjwa wa TB. Ukikubali, mtoto wako atapimwa.

Hiyo itahusisha matembezi 2 kutoka Zahanati ya Kifua ya RAH (siku 3 tofauti), kwanza kumpa Kipimo cha Ngozi cha Kifua Kikuu na tena kupima matokeo yake. Wanafunzi ambao wamekuta TB wanahitaji mfululizo wa tiba ya vidonge. Huduma zote ni bure.



Tembezi 1 – Kipimo cha Ngozi ya Kifua Kikuu



Tembezi 2 – Kupima matokeo yake

Utaratibu wa Shule

Matazamio ya Matendo

Shule ina kanuni ya matendo ambayo wanafunzi wanatazamiwa kufuata. Matendo yanayoheshimu haki ya wanafunzi kujifunza na haki ya walimu kufundisha ni matendo yenye wajibu.

Kujifunza kunasaidiwa wakati wanafunzi:

- Wapo salama na wa hakika
- Wanahisi wapo mahali pake na kutunzwa
- Wanatambuliwa kama watu muhimu
- Wanaheshimu utofauti wa kitamaduni na kidini
- Wanaweza kuamua maamuzi mazuri na uchaguzi mzuri
- wanafurahisha shuleni
- wanafanikia mafaniko.

Walimu na wanafunzi wanatunga masharti ya darasa pamoja. Matendo yasiyofaa darasani yanaweza kutokea:

- kumbusho ya sharti na mazungumzo.
- 'kipindi cha kutengwa' darasani
- 'kipindi cha kutengwa' kwa darasani lingine
- 'kipindi cha kutengwa' pale ofisini.

Kiwanjani, kuna masharti ya kawaida ambayo wanafunzi wote wafuate. Ikiwa sharti likivunjika, wanafunzi wanaweza kupata haki yao kucheza kuachwa. Wanahitajika kuketi bila kucheza na kufikiria kuhusu matendo yao.

Ikiwa matendo ya mwanafunzi ni mno au hayafai kila mara, shule zinaweza:

- Kuwasiliana nyumbani na kupanga mkutano na walezi
- Kutumia anuwai ya matokeo ya kufaa
- Kumsindikiza mwanafunzi kwake au kumsimamisha kwa muda/kumtenga shuleni.

Adabu ya viboko, kama kupiga, kupiga na fimbo au kufinya haitumiki kamwe. Ufahamu wa mwanafunzi wa mtazamio ya matendo na matokeo yake yanasaidiwa na ushauri nasaha, kuonyesha mtindo na kuimarisha matendo yenye kufaa.

Maktaba

Wanafunzi wanaweza kukopa vitabu kutoka maktaba kuchukua kusoma nyumbani. Virudishwe baada ya:

- wiki 1.
 wiki 2.

Tafadhali usiandike ndani kitabu cha kusomea. Ikiwa kitabu kinapotezwa au kuharibika, unaweza kuombewa kukilipa.

Vitu vya Thamani

Inashauriliwa kwamba watoto wasilete vitu vya thamani shulene, km. simu ya mkononi, iPods na kiasi kikubwa cha pesa.

Shule haihusiki kwa kupotezwa kokote.



Haki ya Wanafunzi Kujifunza



Haki ya Wanafunzi ya Kuhisi Salama na Hakika

"Kipindi cha Kutengwa"



Maktaba ya Shule

Mali Iliyopotezwa

Ikiwa mtoto wako akipoteza yoyote ya mali yake shuleni, anaweza kuitafuta katika sanduku la mali iliyopotezwa:

- katika ofisi ya mbele.
- katika kantini.
- nje ya ofisi ya IELC.
- ndani maktaba.
- katika JP eneo la kuchezea ndani.
- nje ya ofisi ya mshauri.



Sanduku la Mali Iliyopotezwa

Kuweka Lebo

Tafadhali hakikisha mali yote ya mtoto wako ina lebo na jina lake, km sanduku la chakula, vyupa vya kinywaji na nguo.

Kanuni ya Kuvaa

Inatazamiwa kwamba wanafunzi watavaa yunifom ya shule kila siku. Waweza kununua yunifom:

- pale shuleni.
- kwa duka la yunifom mjini.
- kwa Big W, Kmart au Target.

Ni muhimu kuwa wanafunzi wavae wa kufaa kwa hali ya hewa ya siku, km sweta, suruali ndefu na viatu vilivyofungwa wakati hali ya hewa ni baridi na kunyenyesha mvua.

Kofia

Tuna siasa ya jua inayohitajika kuvaa kofia ya shule. Ikiwa mtoto hana kofia ataketi katika eneo la kivuli.

Kofia ibaki shuleni na ivaliwe wakati wowote yupo nje:

- wakati wowote mnamo mwaka.
- wakati wa muhula 1 na muhula 4.
- wakati wa muhula 1, 3 & 4 na muhula 2 wakati UV ni juu zaidi ya 3.
- wakati wa muhula 1, 3 and 4.
- wakati wowote mnamo mwaka – wakati kiwango cha UV ni 3 na juu zaidi.

Kofia ya Shule

Ikiwa mtoto wako anapoteza kofia yake utahitaji kuinunua nyingine kutoka ofisi ya mbele.

Nguo zenye Kufaa Shuleni

Nguo za Juu



Polo ya Shule



Sweta ya Shule



T Shati ya Shule

Nguo za Chini



Suruali Ndefu



Captura

Gauni



Gauni ya Shule

Chakula na Ulisha Bora

Kipindi cha Kupumzika

Watoto wanaleta kumbwe kidogo shuleni kwa kipindi cha kupumzika km matunda. Tunatia moyo watoto kuleta chapa cha maji kunywa kila siku.

Kipindi cha Chakula cha Mchana

Watoto wanahitaji kuleta chakula chao cha mchana kutoka nyumbani. Tunaomba wanafunzi kuleta chakula bora shuleni. Tafadhali usipeleke pipi, vinwaji vya soda, ubani nk.

- Pia wanaweza kuagiza chakula kutoka kantini. Ni wazi:
- kila siku
 - Jumanne na Jamatano (Tuesday na Wednesday)
 - Jumanne hadi Ijumaa (Tuesday hadi Friday).
- Pia wanaweza kuagiza chakula kutoka duka la mtaa.
- Watoto wanaandika agizo lao kwenye begi la chakula ambalo limetolewa na shule na kuweka pesa ndani begi.

Hatuwezi kupasha chakula kilicholetwa kutoka nyumbani.

Mzio

Kwa sababu kuna wanafunzi wanaokuwa na mzio wa karanga, usilete chakula kinachokuwa karanga au kasheshe ndani shuleni, km muesli bars, nutella, sorsi ya karanga.



Mawazo ya Kumbwe yenye Afya



Mawazo ya Chakula chenye Afya cha Mchana

Kuhusisha Wazazi

Tunakaribisha ushiriki wa wazazi/ walezi katika maisha ya shule. Msaada huu unaweza kutokea kwa njia nyingi km kusikiliza watoto wanaposoma, kusaidia kwa matembezi, kusaidia katika vipindi vya shughuli nk. Umwone mwalimu wa mtoto wako kama ukitaka kusaidia shuleni.

Tafadhali angalia begi ya mtoto wako kila jioni kwa mawasiliano yafuatayo.

Vitabu vya Kusomea

Vitabu vya kusomea vitakuja nyumbani kila siku. Ni muhimu kwamba mtoto wako asomee kwa mtu kila jioni. Tafadhali hakikisha kitabu cha kusomea cha mtoto wako kiende tena shuleni kila siku.

Kazi za Nyumbani

Matazamio ya kazi za nyumbani yanabadili. Walimu wanafikiria umri, uwezo, daraja la Kiingereza la mtoto, msaada wa familia na rasilimali. Ikiwa kuna mashaka yoyote kuhusu kazi za nyumbani uongee na mwalimu wa mtoto wako.

Barua za habari na Kumbusho

Barua ya habari inatumia nyumbani:

- kila wiki ya pili.
- kila mwezi.
- mara mbili kila muhula.
- mara 3 kila muhula.

Karatasi nyingine zinaweza kutumiwa nyumbani pia kuhusu matembezi, siku za kumaliza mapema, muda wa kufunga shule nk.

Karatasi nyingine zinaweza kuhitaji sahihi kabla kurudisha shuleni.

Vitabu vya Kumbukumbu/ Mawasiliano

Wakati wengine mwalimu wa mtoto wako anaweza kuandika kumbusho kwa wewe katika kitabu chake cha mawasiliano au cha kumbukumbu. Wewe pia unaweza kuandika maandishi kwa mwalimu wa mtoto wako.


Wanafunzi wanatumia vitabu vyao vya kumbukumbu kuandika kazi zao za nyumbani na mambo mengine kukumbuka. Hayo yanahitaji sahihi mwisho wa wiki.

Kitabu cha
Kumbukumbu cha
Mawasiliano

Kutoa Ripoti kwa Wazazi/ Walezi

Walimu watatoa ripoti kuhusu maendeleo ya mtoto wako kujifunza.

- Mahojiano ya mzazi/mwalimu/mwanafunzi yanatokea mnamo mwaka. Wakalimani wanapatikana wanapohitajika.
- Ripoti ya maandishi inapeleka nyumbani wakati mtoto wako anapoondoka mradi.
- Kupiga simu na miadi mingine inapangaliwa, inapohitajika.



Ada za Shule

Ada za shule zinabadilika shule kwa shule. Ada za Shule (au 'Malipo ya Vifaa na Huduma ya Shule') zimewekwa na Baraza ya Uongozi na zinalipa kwa vifaa vya kuandika, vifaa vyenye kuchapishwa, vifaa vya sanaa na kazi za mkono na kutumia huduma kama maktaba, vifaa vya teknolojia na mchezo.

Kadi ya Shule

Ikiwa una Kadi ya Kipunguzo cha Centrelink, familia yako inaweza kupata msaada wa kipesa kutoka serikali. Msaada huu unaitwa **Kadi ya Shule**.

Kadi ya Shule inatumiwa kulipa gharama ya Malipo ya Vifaa na Huduma ya Shule. Hailipi kwa uniform ya shule, matembezi au matukio maalum.

Ikiwa una kadi, tafahali ulete Kadi yako ya Kipunguzo cha Centrelink pamoja na viza yako shuleni mapema iwezekanavyo.



Orodha ya Kurasa

	Nambari ya Kurasa
Habari za Kuwasiliana na Shule	1
<i>Kuhusu Mradi Makini wa Lugha ya Kiingereza na Mradi wa Wapya Waliowasili katika Australia Kusini</i>	2
Sababu	2
Muda wa Kukaa	3
Kuwakwa Darasani	3
Mabadiliko	3
Mtalaa	3
Kufundisha na Kukadiria	3
Maafisa wenye Lugha Mbili wa Huduma za Shule	4
Matembezi na Matukio ya Shule	4
Usafiri	4
Habari za Shule	4
Wakati wa Shule	4
Wakati wa Kengele	4
Mahudhurio/Kutokuwepo	5
Kuchelewa Kuja au Kuondoka Mapema	5
Kusimamia Kiwanjani	5

	Nambari ya Kurasa
Afya na Usalama wa Wanafunzi	5
Mazingira ya Salama wa Mtoto	5
Utaratibu wa Dharura	5
Chawa ya Kichwa	5
Hali ya Hewa ya Joto au yenye Mvua	6
Kuumwa/Jeraha	6
Magonjwa ya Kuambukiza	6
Madawa	6
Huduma ya Meno ya Shule	7
Kupima Kifua Kikuu	7
Utaratibu wa Shule	8
Matazamio ya Matendo	8
Maktaba	8
Vitu vya Thamani	8
Mali Iliyopotezwa	9
Kuweka Lebo	9
Kanuni ya Kuvaa	9
Kofia	9
Nguo za Kufaa Shuleni	9
Chakula na Ulishe Bora	10
Kipindi cha Kupumzika	10
Kipindi cha Chakula cha Mchana	10
Mzio	10
Kuhusisha Wazazi	10
Vitabu vya Kusomea	10
Kazi ya Nyumbani	10
Barua za Habari na Kumbusho	10
Vitabu vya Kumbukumbu/Mawasiliano	10
Kutoa Ripoti kwa Wazazi/ Walezi	11
Ada za Shule	11
Kadi ya Shule	11